MASWALI YA KUJADILI NA DONDOO (CHOZI LA HERI)

a) MASWALI YA KUJADILI

1) “Mwanamke wa Wahafidhina anakabiliwa na changamoto tele.” Jadili. (alama 20)
2) “Haki za watoto kama vizazi vya kesho zimepuuzwa nchini Wahafidhina.” Unakubali? Jadili (alama 20)
3) Fafanua hoja kumi kuonyesha maafa yanayoweza kusababishwa na ubaguzi. (alama 20)
4) “Riwaya ya Chozi la Heri imejaa kuvunjikiwa.” Eleza. (alama 20)
5) Ni upi msimamo wa mwandishi kuhusu suala la elimu katika Chozi la Heri? (alama 20)
6) “Maisha ni safari isiyo na likizo wala pumziko.” Jadili ufaavu wa kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri. (alama 20)
7) “Mwanamke ametoa mchango mkubwa kuiendeleza jamii yake.” Jadili hoja kumi. (alama 20)
8) “Jamii ya Chozi la Heri imepotea njia.” Jadili. (alama 20)
9) Tetea kauli kwamba ‘matatizo ya Wahafidhina ni msiba wa kujitakia.’ (alama 20)
10) “Vijana ni bomu linaloweza kulipuka wakati wowote ikiwa matatizo yao hayatashughulikiwa.” Toa hoja kumi kuunga mkono usemi huu. (alama 20)
11) Jadili maudhui ya majaaliwa na dini kama yanavyojitokeza katika Chozi la Heri. (alama 20) •
12) “Maisha ya aila ya Lunga ni majaaliwa.” Fafanua. (alama 2)
13) Jadili jinsi wahusika Ridhaa, Mwangeka, na Mwaliko walivyokuza maudhui ya majaaliwa (alama 3)
14) Fafanua jinsi riwaya ya Chozi la Heri ililenga kuiadilisha jamii. (alama 20)
15) “Maisha ya Umulkheri ni kama tiara ipeperushwayo na upepo.” Tetea kauli hii kwa kurejelea hoja mbili.
16) “Jukumu la malezi halifai kuachiwa wazazi tu.” Tathmini uhalisia wa usemi huu huku ukirejelea
17) “Ufisadi ni zimwi linaloweza kuimeza jamii nzima ya Afrika kwa mkupuo mmoja.” Jadili mtazamo huu kwa kurejelea hoja kumi kutoka riwayani. (alama 20)
18) Eleza namna mwandishi alivyofanikiwa kutumia majazi katika kazi yake. (alama 20)

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706

19) “Akikupa kilema hukupa na mwendo.” Eleza uhalisi wa methali hii kwa kurejelea hoja tano kuhusu Lunga baada ya kustaafishwa. (alama 10)
20) Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kitabuni, onyesha jinsi mwandishi alivyofanikiwa kutumia methali, majazi, lakabu na misemo katika kazi yake. (alama 20)
21) Kwa kurejelea hoja kumi, tathmini umuhimu wa barua zilizotumika kitabuni. (alama 20)
22) “Ridhaa ni kielelezo bora cha mwanajamii halisi.” Tetea kauli hii kwa kutoa hoja kumi. (alama20)
23) Jadili athari za ukabila na unasaba katika Chozi la Heri. (alama 20)
24) “Binadamu heshi kuumbwa hadi siku ya mwisho.” Ni vipi methali hii inamfaa Bwana Lunga? (alama 20)
25) Kwa kurejelea wimbo wa Shamsi, fafanua matatizo kumi yanayowakumba vijana wa sasa.” (alama 20)
26) “Anwani Chozi la Heri inafaa.” Eleza kwa kutoa hoja kumi. (alama 20)
27) “Majuto ni mjukuu mwishowe huja kinyume.” Kwa kutaja mifano kumi, jadili ufaafu wa methali hii huku ukirejelea Bwana Lunga na mkewe. (alama 20)
28) “Jamii ya Wahafidhina inahitaji mabadiliko.” Jadili. (alama 20)
29) Fafanua matumizi ya taswira, kinaya, sadfa na utabiri katika riwaya. (alama 20)
30) Fafanua manufaa kumi ya hotuba ya kila Ijumaa ya Lunga kwa wanafunzi wenzake na ile ya Ridhaa kwa Mwangeka wanapokutana katika uwanja wa ndege. (alama 20)
31) “Annatila ni mtoto ambaye huenda angeshuhudia makubwa katika siku zake za usoni ikiwa hangeaga mapema.” Taja hoja kumi. (alama 20)
32) Ni upi mtazamo wa mwandishi kuhusu mashirika ya kijamii? (alama 20)
33) “Ibilisi wa mtu ni mtu.” Jadili ukweli wa methali hii kwa kurejelea riwaya. (alama 20)
34) “Takriban kila tatizo linalokumba jamii lina utatuzi wake.” Jadili hoja kumi kuunga mkono kauli hii.(al 20)
35) Mwalimu Dhahabu ni kielelezo cha walimu wa aina gani? Taja hoja kumi katika jibu lako. (alama20)
36) “Binadamu ni adui wa mwenzake.” Tathmini ufaavu wa kauli hii kwa mujibu wa riwaya. (alama20)
37) “Wahafidhina wana majibu ya matatizo yote yanayowakumba.” Jadili. (alama 20) Tanbihi

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706

38) “Mwandishi wa Chozi la Heri amemkuza mwanamke na kumtweza mwanamume.” Tathmini kwa kutaja hoja kumi. (alama 20)
39) Fafanua matatizo kumi yanayokumba familia ya sasa kwa mujibu wa riwaya. (alama 20)
40) Jadili dhima kumi za hotuba za Ridhaa. (alama 20)
41) “Chozi la Heri ni riwaya ya kitashtiti.” Jadili. (alama 20)
42) Linganisha na ulinganue sifa za Sauna na Fungo. (alama 20)
43) Eleza matumizi ya kisengerenyuma katika riwaya. (alama 20)
44) “Wahafidhina ni watu wa kusikitisha.” Jadili. (alama 20)
45) Jadili athari kumi za utamaduni na ufeministi katika riwaya ya Chozi la Heri. (alama 20)
46) 44. Eleza jinsi Wahafidhina wanavyoweza kukabiliana na matatizo yanayowakumba. (alama 20)
47) Ni kwa kiwango gani nchi ya Wahafidhina inalingana na nchi za Kiafrika? (alama 20) Tanbihi
48) Tambua manufaa kumi ya mbinu ya hadithi ndani ya hadithi katika riwaya. (alama 20)
49) “Jamii ya Chozi la Heri imejuta.” Jadili. (alama 20)
50) Tathmini mchango wa wahusika Neema, Naomi, Ridhaa na Kaizari katika maudhui ya ndoa. (alama 20)
51) Jadili vikwazo kumi vinavyotatiza elimu nchini Wahafidhina. (alama 20)
52) “Riwaya ya Chozi la Heri imemulika uhalisia.” Jadili. (alama 20)
53) Kwa kurejelea mifano kumi, fafanua jinsi nchi ya Wahafidhina ilivyojaa wasaliti. (alama 20)
54) Fafanua matatizo kumi yanayowafika watoto baada ya wazazi wao kuwaondokea. (alama 20)
55) “Kijengacho mtu ni utu.” Ni vipi Wahafidhina walikaidi msemo huu? (alama 20) Tanbihi
56) “Jamii ya Chozi la Heri yafaa ijisake na izaliwe upya.” Jadili. (alama 20)
57) Tathmini jinsi mwandishi wa riwaya alivyodhamiria kujenga jamii mpya yenye matumaini.(alama20)
58) Tathmini jinsi baadhi ya raia nchini Wahafidhina walivyowajibika. (alama 20)
59) Fafanua sababu kumi zinazosababisha uharibifu wa mali nchini Wahafidhina. (alama 20)
60) “Duniani kuna ibilisi na malaika wa heri.” Tathmini. (alama 20)
61) “Hata afanye nini, binadamu hawezi akabadilisha majaaliwa yake.” Jadili. (alama 5)
62) “Misukosuko na mikosi maishani huimarisha hulka ya mtu.” Fafanua. (alama 20)
63) “Raia wa Wahafidhina wanastahili haki.” Eleza. (alama 20)

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706

64) "Jamii ya Chozi la Heri inafaa kusamehewa." Eleza. (alama 20)

b) MASWALI YA DONDOO

1. **"…**mwanangu, mwanamume hufumbika hisia**…Unyonge haukuumbiwa majimbi…"**
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Taja na ueleze mbinu inayorejelewa na maneno yaliyokolezwa rangi. (alama 2)
   c) Jadili maudhui yanayorejelewa na dondoo hili. (alama 14)
2. "…kumbe wewe ni sawa na yule Mwangeka wa kihistoria ambaye kivuli chake kikitembea siku zote mbele…"
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Eleza sifa **nane** za mnenaji. (alama 16)
3. "…umewahi kumwona mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota…"
   a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)
   b) Tambua mbinu iliyotumika katika maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
   c) Eleza sifa **tatu** za msemaji wa maneno haya. (alama 6)
4. "…akaamua kuwahamishia wake wawili wa mwisho Msitu wa Heri…"
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Ni mbinu gani ya uandishi imetumika hapa? (alama 2)
   c) Taja na ueleze matumizi mengine saba ya mbinu uliyoitaja katika (alama14)
5. "…ni vyema kujifunza kuishi na wenzako bila kujali tofauti za ukoo na nasaba."
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Jadili hoja **nane** kuonyesha namna tofauti zilizopigiwa mstari ziliishia kuiporomosha Wahafidhina. (alama 16)
6. "Matrekta ya Baraza la jiji yamefanya kazi ya Waheshimiwa alasiri ya leo."
   a) Fafanua muktadha wa dondoo. (alama 4)
   b) Tambua mbinu iliyotumika. (alama 2)
   c) Fafanua maudhui yanayorejelewa. (alama 4)
   d) Tambua matumizi mengine kumi ya mbinu uliyoitaja katika sehemu ya (b) (alama 10)
7. "Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira."
   a) Fafanua muktadha wa dondoo. (alama 4)
   b) Eleza mbinu iliyotumika. (alama 2)
   c) Fafanua sifa **saba** za mnenaji. (alama 14)
8. "Haiwezekani! Hili haliwezekani! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kile…" (uk. 17)
   a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   b) Jadili maudhui yanayorejelewa hapa. (alama 16)
9. "Tawala Wahafidhina tawala, Mwanzi wetu tawala…"
   a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   b) Ni mbinu gani imetumika hapa? (alama 2)
   c) Eleza matokeo **saba** ya maneno haya. (alama 14)
10. "Mtu anahitimu hata digrii tatu, kisha anapiga lami kwa miaka kumi…"
    a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
    b) Eleza mbinu mbili zinazorejelewa na maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 4)
    c) Eleza maudhui yanayorejelewa na maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 8)

d) Msemaji wa maneno haya anawakilisha watu wenye sifa zipi? (alama 4)

11. "Afadhali *Papa*, amepita hapa mara tatu akatugawia kila mtu shilingi mia mia…"
   a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   b) Tambua mbinu iliyotumika katika neno lililoandikwa kwa italiki. (alama 2)
   c) Tambua maudhui yanayorejelewa na dondoo 73asha utoe mifano mingine **saba** kutoka riwayani.(alama 14)

12. "Wapi kile kidume chako kijoga?"
   a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)
   b) Fafanua mbinu inayorejelewa na maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
   c) Eleza hatima ya maneno haya. (alama 4)
   d) Jadili sifa **tano** hasi za wanenaji wa maneno haya. (alama 10)

13. "…*nikapiga moyo konde* kukabiliana na hali hii mpya."
   a) Tambua muktadha wa dondoo. (alama 4)
   b) Eleza mbinu inayorejelewa na maneno yaliyo katika italiki. (alama 2)
   c) Taja mifano **saba** ya "hali mpya" ambazo mnenaji alikabiliana nazo. (alama 14)

14. "Sandarusi zenyewe mtu anazitafuta kwenye milima ya taka zinazotolewa huko waishio waheshimiwa kuja kutupwa huku."
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Kwa kurejelea mifano mingine **minane**, fafanua maudhui yanayoangaziwa na maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 16) .

15. *"...Nilikuwa na Njaa Ukanilisha…"*
   a) Tambua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Taja na ueleze mbinu ya uandishi iliyotumika hapa. (alama 2)
   c) Toa mifano mingine **minane** ya mbinu hii katika riwaya. (alama 16)

16. "Ningekuwa hasidi wa usawa wa kijinsia nisingewapelekeni nyinyi shuleni."
   a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Fafanua sifa **moja** ya mnenaji inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

17. "Je, binadamu aliandikiwa kumpoka binadamu mwenzake maisha?"
   a) fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Fafanua mbinu iliyotumika kwenye dondoo. (alama 2)
   c) Eleza umuhimu wa mbinu uliyoitaja katika (b) (alama 14)

18. "Jamani injini ya lori hili bado inanguruma na huenda moto ukazuka…"
   a) Weka dondoo katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Tambua mbinu iliyotumika. (alama 2)
   c) Taja mifano zaidi ya mbinu hiyo kutoka riwayani. (alama 14)

19. *"**This country has nothing to offer**."*
   a) Weka dondoo kwenye muktadha wake. (alama 4)
   b) Eleza maudhui yanayorejelewa na dondoo. (alama 4)
   c) Fafanua mifano mingine **kumi na miwili** ya mbinu iliyotumika hapa. (alama12)

20. "Utamwozaje mwanetu kwa mtu wa ukoo ambao huvaa nguo ndani inje?"
   a) Fafanua muktadha wa dondoo. (alama 4)
   b) Taja na ueleze mbinu iliyotumika. (alama 2)
   c) Fafanua athari **saba** za maudhui yanayorejelewa na dondoo. (alama 14)

21. "…wamewaacha wanyama kama mayatima kwa kuwapoka makazi yao."
   a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706

b) Taja mbinu iliyotumika. (alama 2)
c) Fafanua maudhui yanayorejelewa kwa kutoa mifano **saba** kutoka riwayani. (alama 14)

22. "…*kunako matanga kumekufa mtu*. Ulimwengu umenifunza kutumia fursa niliyo nayo kuyaboresha Maisha yangu

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Tambua mbinu inayorejelewa na maneno yaliyoandikwa kwa italiki. (alama 2)
c) Fafanua sifa **moja** ya mnenaji inayorejelewa na maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)
d) Kwa kurejelea hoja **sita**, fafanua jinsi ulimwengu umemfunza msemaji. (alama 12)

23. "Auntie Sauna! Kumbe ile imani na uchangamfu wako na ahadi ya kututunza baada ya kifo cha baba ilikuwa siasa…"
a) Weka maneno haya kwenye muktadha wake. (alama 4)
b) Eleza sifa **tano** chanya za mnenaji. (alama 10)
c) Eleza sifa za Auntie Sauna. (alama 6)

24. "…angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo mbele ya macho ya wanawe…"
a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza sifa **moja** ya mrejelewa kwa mujibu wa dondoo hili. (uk. 2)
c) Kwa kutoa mifano **saba** kutoka kitabuni, eleza maudhui yoyote yanayoangaziwa na dondoo. (alama 14)

25. "…mwanangu, walimwengu ni hasidi. Ndio walionisababishia uwele. Ishi, mwanangu, utawaona."
a) Weka dondoo kwenye muktadha wake. (alama 4)
b) Fafanua jinsi walimwengu walivyo "hasidi" kwa kurejelea mnenaji na aila yake.(alama 10)
c) Tambua mbinu inayoangaziwa na maneno yaliyopigiwa mstari kisha utoe mifano mingine kutoka kitabuni. (alama 6)

26. "…jambo la sudi huenda kwa sudi."
a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)
b) Ni mbinu gani imetumika hapa? (alama 2)
c) Fafanua uhalisia wa mbinu uliyotaja kwa Ridhaa na wana wa Lunga. (alama 14)

27. "…walikuuza kwangu ili wapate pesa za kuwasomeshea ndugu zako watano wa kiume?"
a. Weka maneno haya kwenye muktadha wake. (alama 4)
b. Fafanua maudhui yanayoangaziwa hapa kwa kurejelea hoja **nane** kutoka riwayani. (alama 16)

28. "…aliniwahi nishai zikiwa zimenilemea, yakatokea ya kutokea…"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Taja na ueleze mbinu iliyotumika. (alama 2)
c) Eleza sifa **tano** za mnenaji kisha ueleze umuhimu wake. (alama 14)

29. "…nilijiona kama *aliyepigwa pute* na dunia."
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Eleza mbinu inayorejelewa na maneno yaliyoandikwa kwa italiki. (alama 2)
c) Rejelea hoja **saba** kudhihirisha kuwa mnenaji amepigwa pute na dunia. (alama 14)

30. "Vuuuk! Engineer Vuuuk! Engineer Vukuto!"

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza mbinu **mbili** zilizotumika katika dondoo. (alama 2)
c) Eleza sifa **nne** chanya za msemewa. (alama 8)

31. "Aah! Kufa mwana kufa…"
a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
b) Eleza mbinu **mbili** zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)
c) Jadili matatizo **sita** yanayomkumba msemaji wa maneno haya. (alama 12)

32. "Nyota yangu ilizimika…"
a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Taja mbinu iliyotumika. (alama 2)
c) Eleza jinsi wahusika hawa walizimikiwa na nyota zao: Chandachema, Zohali, Lime, na Sauna. (alama 14)

33. "Hakuna amani bila kuheshimu mwanamume. Hatuwezi kukubali haya. Hata mizimu itatucheka!"
a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
b) Taja na ueleze mbinu **mbili** zilizotumika katika dondoo. (alama 4)
c) Jadili maudhui yanayorejelewa na dondoo. (alama 12)

34. "Dickson, wewe jikaze. Mzee wako hayupo hapa, amejipumzikia ahera."
a) Weka dondoo hili kwenye muktadha wake. (alama 4)
b) Eleza sifa **mbili** hasi za Dickson. (alama 4)
c) Jadili maudhui yanayorejelewa na maneno yaliyopigiwa mstari kwa kufafanua mifano **sita** kutoka kitabuni. (alama 12)

35. "Tusije tukawa sawa na yule mtumishi kwenye kitabu kitakatifu ambaye alichimbia talanta chini badala ya kuizalisha!"
a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Eleza mbinu **mbili** zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)
c) Fafanua sifa **sita** chanya za mnenaji. (alama 12)

36. "…ingawa tulitangaziwa kuwa msitu huu ni marufuku kwa binadamu, usiku wa manane husikika milio
a) Weka maneno haya kwenye muktadha wake. (alama 4)
b) Tambua mbinu **mbili** zilizotumika kwenye dondoo. (alama 4)
c) Jadili maudhui yanayojitokeza katika dondoo kwa kurejelea mifano mbalimbali. (alama 12)

37. "Maskini ndugu yangu mdogo!... Binadamu waliwasongomezea wapi?"
a) Tambua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza sifa **nne** za mzungumzaji. (alama 8)
c) Jadili mchango wa mnenaji katika maudhui ya elimu na ndoa.(alama 8)

38. "…wazazi wako walafi walikuuza kwangu ili wapate pesa za kuwasomeshea ndugu zako watano wa kiume?"
a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Jadili maudhui **mawili** yanayoangaziwa na maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 16)

39. "This is a nest. I cannot live here, not now, not ever."
a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
b) Tambua mbinu **mbili** zilizotumika. (alama 4)

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706

c) Eleza sifa **mbili** za mnenaji. (alama 4)
d) Taja mifano mingine ya mbinu ulizotambua hapo juu. (alama 8)

40. "…mara ngapi umeponea tundu la sindano kunaswa na mashine za forodha? Je, *isingekuwa mwajiri wako kuvilainisha viganja vya maafisa wa forodha,* wewe na wenzako msingekuwa mmeozea kwenye magereza…"
a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Kwa kurejelea mifano mbalimbali, eleza athari **nane** za maudhui yanayorejelewa na maneno yaliyo kwenye italiki. (alama 16)

41. "…misafara ya watu waliohama kwao…"
a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
b) Taja sababu **mbili** zilizosababisha hali hii. (alama 4)
c) Jadili maudhui yaliyo katika dondoo. (alama 12)

42. "…wewe jikaze. Mzee wako hayupo hapa, amejipumzikia ahera."
a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Mrejelewa anajikaza dhidhi ya nini? (alama 2)
c) Eleza sababu **saba** zilizosababisha wahusika mbalimbali "kujipumzikia ahera." (alama 14)

43. "…simtaki huyo Kiboko, namtaka Papa. Kiboko hata chumvi hatoi. Afadhali Papa, amepita hapa *mara tatu* akatugawia kila mtu shilingi mia mia…"
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Fafanua mbinu inayoangaziwa na manenо yaliyo katika italiki. (alama 2)
c) Jadili maudhui yoyote yanayoangaziwa na dondoo kwa kutaja mifano **saba** kutoka kitabuni. (alama 14)

44. "Mwangeka na Mwangemi walilazimika kulala njaa kama adhabu kutoka kwa wazazi wao kwa kumwiga babu…"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Jadili maudhui yanayojitokeza katika dondoo. (alama 16)

45. "Hili ni wingu la kupita…halipaswi kumtia mkulima matumaini…"
a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Tambua mbinu iliyotumika hapa. (alama 2)
c) Fafanua matumizi mengine ya mbinu uliyoitaja hapo juu. (alama 14)

46. "Utamwozaje mwanetu kwa mtu wa ukoo ambao huvaa nguo ndani inje?"
a) Tambua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Fafanua mbinu yoyote **moja** iliyotumika hapa. (alama 2)
c) Jadili matumizi mengine **saba** ya mbinu uliyoitaja. (alama 14)

47. "Wasichana wengi huozwa au kuolewa kwa hiari mara wanapopashwa tohara."
a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Kando na kuozwa na kupashwa tohara, fafanua dhuluma nyingine **nane** anazopitia mtoto wa kike katika ukuaji wake. (alama 16)

48. *"…mashamba* ***makubwamakubwa****…"*
a) Weka maneno haya kwenye muktadha wake. (alama 4)
b) Tambua mbinu inayorejelewa na maneno yaliyokolezwa rangi. (alama 2)
c) Taja matumizi mengine ya mbinu hiyo. (alama 14)

49. "…hata mtu akijitia wasiwasi vipi, hawezi kuongezea hata pima moja katika maisha yake…"
a) Weka dondoo hili kwenye muktadha wake. (alama 4)
b) Fafanua sifa **tatu** za mnenaji. (alama 6)

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706

c) Jadili maudhui yanayorejelewa na dondoo. (alama 10)

50. "…ukimlea wako na wa mwenzio mlee."

a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Tambua mbinu ya lugha iliyotumika. (alama 2) .

c) Jadili jinsi wahusika mbalimbali walivyozingatia ujumbe wa maneno hayo. (alama 14)

51. "…**walikita ardhini kama mikuki** iliyochomekwa hapo…"

a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b) Tambua mbinu inayorejelewa na maneno yaliyokolezwa rangi (alama 2)

c) Eleza matumizi mengine **saba** ya mbinu uliyoitaja hapo juu. (alama 14)

52. "Nyinyi ndio mlioturudisha nyuma miaka yote hii. Mnatuhadaa kwa vishahada mnavyotupa vyuoni, vishahada ambavyo ni laana kwetu…"

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Fafanua sifa **tatu** hasi za mnenaji. (alama 6)

c) cJadili hoja **tano** kuonyesha kuwa visha~~h~~ada vinavyopeanwa vyuoni ni laana. (alama 10)

53. "…baada ya kiza kizito huja mawio ya uzawa wa jamii mpya yenye matumaini."

a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Kwa kurejelea mifano **minane**, onyesha kuwa riwaya hii ni mawio ya uzawa wa jamii mpya yenye matumaini. (alama 16)

54. "Wewe ni *Mfuata Mvua*."

a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b) Jadili sifa **mbili** za mrejelewa. (alama 4)

c) Jadili mifano mingine **sita** ya mbinu iliyotumika kwenye dondoo. (alama 12)

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA NAMBARI 0724351706

Pia kuna maswali na majibu ya kigogo,tumbo lisiloshiba,fasihi simulii,insha,ushairi na isimujamii